**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MAADHIMISHO YA UZINDUZI WA JIMBO JIPYA LA BAGAMOYO NA KUSIMIKWA K WA ASKOFU WAKE WA KWANZA, MHASHAMU ASKOFU STEPHANO LAMECK MUSOMBA (OSA)

**BAGAMOYO, PWANI**

**04 MEI 2025**

- ***Mhashamu Askofu Mkuu Angelo Accattino, Apostolic Nuncio to Tanzania;***
- ***Mhashamu Askofu Thaddaeus Ruwa'ichi, OFMCap, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam;***
- ***Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam;***
- ***Mhashamu Askofu Stephano Lameck Musomba, OSA, Askofu wa Kwanza wa Jimbo Katoliki la Bagamoyo;***
- ***Wahashamu Maaskofu Wakuu na Wahashamu Maaskofu mliopo;***
- ***Mhe. Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote mliopo;***
- ***Mhe. Shaibu Ndemanga, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo na Wakuu wa wilaya wote mliopo;***
- ***Waheshimiwa sana Mapadre, Mashemasi na watawa wote;***
- ***Wahe. viongozi wa dini mbalimbali mliopo;***
- ***Viongozi wa Vyama vya Siasa;***
- ***Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Pwani;***
- ***Waamini wenzangu na watu wote wenye mapenzi mema;***

**Tumsifu Yesu Kristo!**
**Jubilei 2025....Mahujaji wa Matumaini!**
**Mungu ni Mwema.....!**

Kanisa Katoliki Tanzania liko katika shamrashamra za uzinduzi wa Jimbo jipya la Bagamoyo uliofanyika jana Jumamosi, Mei 3, 2025; na hivi leo kusimikwa rasmi Askofu wake wa Kwanza, Mhashamu Askofu Stephano Lameck Musomba, Mtawa wa Shirika la Mt. Agustino (OSA). Awali ya yote, napenda kuwaletea salamu na pongezi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maadhimisho haya. Mhe. Rais alipokea na kuridhia ombi lenu kuwa mgeni rasmi. Hata hivyo, kutokana na majukumu mengine ya kitaifa aliyonayo, amenituma nimwakilishe. Nami nilifurahia sana upendeleo wa kuja kuungana na kanisa katika maadhimisho haya yenye baraka na furaha kubwa. Mhe. Rais anakupongeza sana Mhashamu Baba Askofu Musomba, kwa kuteuliwa na Hayati Papa Francis kuwa Askofu wa kwanza wa Jimbo jipya la Bagamoyo na kwa kusimikwa rasmi katika nafasi hiyo siku ya leo. Aidha, Rais analipongeza Kanisa Katoliki kwa uzinduzi wa Jimbo jipya, pamoja na Waheshimiwa Mapadre na Watawa wote watakaohudumu katika Jimbo hili jipya.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***

Nami naungana na Mhe. Rais, kuwapongeza wanajimbo la Bagamoyo kwa kupata Jimbo na Mchungaji Mkuu. Kama ambavyo imeelezwa, Bagamoyo imekuwa ndiyo mlango wa kuingia kwa imani ya kikristo hapa nchini na maeneo mengine ya Afrika Mashariki na Kati. Kwa historia yake, pengine Bagamoyo ilistahili kuwa Jimbo muda mrefu uliopita. Lakini kama maandiko matakatifu yanavyosema, kila jambo na wakati wake (Mhubiri 3: 1-8). Hivyo, tuzidi kumshukuru Mungu kwa kuruhusu jambo hili litimie katika mwaka huu wa Bwana. Vilevile, kwa namna ya pekee kabisa nami naomba kukupongeza sana, Mhashamu Askofu Musomba, kwa kusimikwa kuwa Askofu wa Kwanza wa Jimbo jipya la Bagamoyo. Jukumu

hili la kichungaji la kulea Jimbo Katoliki la Bagamoyo ni kubwa, lakini Mungu aliyekuita katika utume na uinjilishaji, atakuwezesha kulitimiza kusudi la wito wako katika Kristo Yesu. Tunasoma katika Waraka kwa Waebrania (Ebr. 5:4) "...*Na hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni"*. Vivyo hivyo, nawapongeza wanajimbo la Bagamoyo kwa kumpata Mhashamu Baba Askofu Musomba, kama kiongozi wenu Mkuu. Ni matumaini yangu kuwa mtampatia ushirikiano wa kutosha, pamoja na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kuwaongoza vema.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Uamuzi wa Baba Mtakatifu Francis kuunda Jimbo hili jipya, si tu umeipa Bagamoyo hadhi, lakini pia umesogeza huduma za kichungaji kwa waamini na utaongeza kasi ya uinjilishaji. Bila shaka kusogea kwa huduma za kichungaji kutaongeza pia upatikanaji wa huduma za kijamii zinazotolewa na Kanisa. Kwa niaba ya Mhe. Rais, napenda kuwahakikishia waamini wa Jimbo Katoliki la Bagamoyo na Watanzania wote kuwa Serikali inathamini sana mchango mkubwa wa Kanisa Katoliki na madhehebu mengine ya dini katika kuimarisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za jamii, hususan afya na elimu. Aidha, Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa viongozi wa dini na taasisi zake ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kuhudumia umma wa watanzania. Kwa maneno mengine, tutazingatia rai iliyotolewa kwamba Serikali iendelee kuunga mkono juhudi za kanisa na kutoa ushirikiano kama mshirika mwenza na si mshindani katika kuwaletea maendeleo Watanzania kwa kuzingatia mazingira mahalia.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***
Tunapoendelea kumshukuru Mungu kwa kutujalia Jimbo jipya la Bagamoyo na kutupatia Mhashamu Baba Askofu Musomba kama mchungaji wetu mkuu, napenda kutumia fursa hii kutilia mkazo, japo kwa kifupi, mambo yafuatayo:

***Kwanza,*** napenda kwa niaba ya Serikali, kutoa pole kwa Padre Dkt. Charles Kitima, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Baraza zima la Maaskofu na Kanisa kwa ujumla, kufuatia tukio la kushambuliwa na kuumizwa vibaya wakati akiwa kwenye makazi yake. Serikali inalaani vikali na kukemea tukio hilo, pamoja na matukio mengine kama hayo ya uvunjifu wa sheria. Napenda niwahakikishie Watanzania na wapenda haki, amani na usalama wote, kuwa tayari Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani imeviagiza vyombo vya dola kuwatafuta, kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria wahusika wa tukio hilo, na wale wote watakaothibitika kuhusika na matukio kama hayo ambayo hayakubaliki kabisa mahali popote. Nawaomba sana Wahashamu Maaskofu, Wakleri na wote walioumizwa na tukio hili baya kujikabidhi kwa Mungu pale tunapoumizwa na udhalimu, kama tunavyosoma katika Waraka wa Kwanza wa Petro (1 Pet. 2:19 ) "*...maana huu ndiyo wema hasa, mtu akivumilia huzuni kwa kumkumbuka Mungu pale ateswapo isivyo haki"* Aidha, nawasihi sana Watanzania tuendelee kupendana na kusimama pamoja kulaani matendo hayo mabaya yasiyoakisi Tanzania yetu inayosifika kama kisiwa cha amani.

***Pili,*** ni wito wa Serikali kwa Watanzania wote kujitokeza kuhuisha taarifa zao katika daftari la kudumu la wapiga kura na kushiriki kikamilifu katika uchaguzi kwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, kushiriki kampeni na kujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi. Aidha,

napenda kusisitiza umuhimu wa kudumisha amani na utulivu wakati wote wa maandalizi na kampeni za uchaguzi mkuu. Ni muhimu pia kuepuka kauli za kibaguzi, kichochezi, uzushi na upotoshaji kupitia mitandao ya kijamii na njia nyingine za mawasiliano kwa misingi ya tofauti ya itikadi zetu za kisiasa, kidini, kabila au rangi. Nawaomba sana waamini wenzangu na Watanzania wote kuzingatia maandiko matakatifu yanayotuasa kuitafuta amani, kama tunavyosoma katika Waraka wa kwanza wa Mtume Petro (1 Pet. 3:11) *"...na aache mabaya, atende mema; atafute amani, aifuate sana."* Katika hili, tujitahidi pia kujizuia na hasa kuzuia ndimi zetu, kama Waraka wa Yakobo (Yak. 1: 19 – 20) unavyotuelekeza kwamba *"...hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi: basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema, wala kukasirika. Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu."* Tukumbuke kwamba amani yetu haina mbadala, hivyo ni wajibu wetu sote kulinda amani na utulivu wa nchi yetu. Napenda kuwaasa vijana kutokubali kutumiwa na wanasiasa wenye uchu wa madaraka, walio tayari kuwatumia kuchochea vurugu wakati wa uchaguzi kwa manufaa yao wenyewe. Napenda pia kuwasisitiza watendaji Serikalini kutenda haki katika utekelezaji wa majukumu waliyokabidhiwa.

Vilevile ni muhimu kuendelea kuliombea Taifa letu kwa Mwenyezi Mungu ili liwe na amani na utulivu, hususan mwaka huu tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Wageni Waalikwa;***

Napongeza homilia nzuri iliyosheheni mafundisho ya msingi kwetu sote iliyotolewa na Mhashamu Askofu Lazarus Msimbe wa Jimbo Katoliki Morogoro, Nimepokea pia risala ya Kanisa iliyosomwa mbele yetu. Aidha, nimepokea ombi mahsusi la Kanisa la kurejeshewa Ardhi ya Bodi ya Wadhamini ya Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro (sasa ni sehemu ya Jimbo Jipya la Bagamoyo), ambayo kwa sasa ni sehemu ya Chuo cha ADEM. Kwa kuwa madai haya yamekuwepo kwa muda mrefu, ni wakati muafaka sasa yakapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kwa ajili hiyo, naelekeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuunda Timu Maalum itakayoshirikisha wataalam kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kukaa mezani na Uongozi wa Kanisa Katoliki Jimbo la Bagamoyo, ili kujadili na kutoa mapendekezo ya namna ya kufikia ufumbuzi wa suala hili. Aidha, Taarifa ya Timu hiyo ya pamoja iwasilishwe Serikalini mapema iwezekanavyo kwa ajili ya uamuzi.

Mwisho, kwa niaba ya Mhe. Rais aliyenituma kumwakilisha katika maadhimisho haya, narudia tena kumpongeza sana Mhashamu Askofu Stephano Musomba, OSA, kwa kusimikwa kwa kuwa Askofu wa kwanza wa Jimbo hili. Aidha, ninamtakia Mhashamu Baba Askofu Musomba afya njema na umri mrefu ili aendelee kutubariki, kutufundisha na kutuombea. Vilevile, ninawatakia waamini wa Jimbo Katoliki la Bagamoyo, wananchi wa Bagamoyo na wote wenye mapenzi mema, heri katika uzinduzi wa Jimbo jipya la Bagamoyo. Naomba nimalizie hotuba hii kwa kukabidhi Sh. Milioni Ishirini (20,000,000) kwa Baba Askofu Musomba kwa ajili ya mafuta ya gari ya kuanzia ziara zake za kichungaji katika Jimbo hili jipya.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**